

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAULI YA WILAYA YA KILOLO

SHULE YA SEKONDARI DABAGA
S. L. P. 285
IRINGA.
14/12/2020.
SIMU; 0759 220 451.

Kumb Na. D.S.S./Adm/Jl/2021.

Kwa Mwanafunzi

S. L. P.

Ndugu,

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI DABAGA WILAYA YA KILOLO
MKOA WA IRINGA MWAKA 2021.**

1.0 UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kijiunga kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021. Shule ya sekondari Dabaga ipo katika kijiji cha Kidabaga, kata ya Dabaga, tarafa ya Kilolo. Umbali wa kilometra 18 mashariki mwa makao makuu ya Halmashauli ya Wilaya ya Kilolo. Usafiri wa basi kutoka Iringa mjini hadi Kidabaga unapatikana katika kituo cha mabasi cha Mlandege au Ipogolo, nauli ni Tsh. 3000/=. Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe 11 Januari 2021, na mwisho wa kuripoti ni tarehe 24 Januari 2021.

2.0 SARE ZA SHULE

(A) WAVULANA

- (i) Suruali mbili (02) rangi kijani jeshi nzito. Mshono; chini upana inchi 14 wenyе mkunjo ('turn up'), yenye marinda mawili (02) na mfuko wa nyuma usiwe na zipu.
- (ii) Mkanda mweusi wa suruali upana inchi 2 wenyе luksi, usiwe na nembo yoyote.
- (iii) Mashati mawili (02) meupe mikono mirefu.
- (iv) Tai rangi kijani jeshi nzito, moja (01).
- (v) Viatu vyeusi nya ngozi vyenye kamba, visivyo na visigino virefu, pea mbili (02).
- (vi) Sweta rangi ya bluu nyeusi ('dark blue') yenye (V) upande wa mbele angalau moja (01)
- (vii) Soksi nyeusi pea mbili (02).
- (viii) 'Track suit' nyeusi yenye mistari myeupe pea moja (01).
- (ix) Kiatu cha michezo pea moja (01).
- (x) 'Shamba dress' suruali rangi ya bluu nyeusi ('dark blue') moja. Mshono zingatia namba (i) hapo juu.
- (xi) 'T-shirt' rangi ya bluu ('blue') inapatikana shulenii.

(B) WASICHANA

- (i) Sketi mbili (02) ndefu zinazoficha soksi rangi kijani jeshi nzito. Mshono: Yenye marinda kumi (10) ya kupanga, mfuko upande wa kushoto, mkanda inchi mbili (02).
- (ii) Mashati mawili (02) meupe mikono mirefu.
- (iii) Tai rangi kijani jeshi nzito, moja (01).
- (iv) Viatu vyeusi nya ngozi vyenye kamba, visivyo na visigino virefu pea mbili (02).
- (v) Sweta rangi ya bluu nyeusi ('dark blue') yenye (V) upande wa mbele angalau moja (01).
- (vi) Soksi nyeupe pea mbili (02).
- (vii) 'Track suit' nyeusi yenye mistari myeupe pea moja (01).
- (viii) Kiatu cha michezo pea moja (01).
- (ix) 'Shamba dress' gauni rangi ya bluu nyeusi ('dark blue') moja. Mshono; Solo, ndefu inayoficha soksi.
- (x) 'T-shirt' rangi ya bluu ('blue') inapatikana shuleni.

ZINGATIA:

1. Rangi ya sare ya shule tumia vielelezo vilivyoambatanishwa katika fomu hii.
2. Mwanafunzi hataruhusiwa kuva nguo nyingine nje ya sare za shule. Hivyo, asije na nguo nyingine nje ya maelekezo haya, atakaguliwa.
3. Mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni akiwa amevaa sare ya shule tayari kwa kuanza masomo.

3.0 MAHITAJI KWA WANAFUNZI WOTE

- a) Bunda moja la karatasi (Rimu A4-Dolphin).
- b) 'Graph Paper'(01).
- c) Daftari 10 (*Counter Book Quire Z*).
- d) 'Mathematical Set'(Mkebe 01).
- e) 'Four figure'(01).
- f) Kamusi/'Dictionary'.
- g) Peni kumi (10).
- h) Rula moja (01).
- i) Penseli tano (05).
- j) Vifaa nya chakula; (Sahani, Bakuli, Kijiko, na Kikombe).
- k) Begi la kubebrea madaftari.
- l) Kwanja ('Slasher') moja (01).
- m) Mfagio ('Soft Broom').
- n) Ndoo lita kumi. (01).
- o) Jembe moja (01) lenye mpini.

4.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenyeye dhamana ya Elimu nchini na ofisi ya Rais-TAMISEMI yenyeye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa shule. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shulenii;

- a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- b) Mahudhurio mazuri katika kila Shughuli ndani na nje ya darasa kulingana na ratiba ya shule ni muhimu.
- c) Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (*'Night Preparation'*).
- d) Kuwahi katika shughuli za shule na nyngine utakazopewa.
- e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
- g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
- h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
- i) Kuthamini mali ya umma. Endapo mwanafunzi atasababisha uharibifu wowote wa mali ya shule/umma, Mzazi/Mlezi atawajibika kulipa.

4.0 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUKUSABABISHA UKAFUKUZWA SHULE

- a) Wizi.
- b) Uasherati, ubakaji na ushoga.
- c) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyta kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi na kubeli.
- d) Makosa ya jinai.
- e) Kupigana au kupiga.
- f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
- g) Kudharau kwa makusudi bendera ya taifa.
- h) Kuoa au kuolewa.
- i) Kupata mimba na kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
- j) Kutoa mimba.
- k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
- l) Kukataa adhabu kwa makusudi.
- m) Kuwa na simu ya mkononi au laini.

Zingatia: Mzazi/mlezi hakikisha umemkagua mwanao na kujiridhisha kuwa hana simu au laini kabla ya kuripoti shulenii.

5.0 MAMBO MENGINE MUHIMU

- A. *'Medical Examination Form'* ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali, na fomu hii itakabidhiva kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shulenii.
- B. Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
- C. Fomu ya wazazi kukiri kukubaliana na sheria na kanuni za shule, pamoja na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

6.0 TAFADHARI SOMA KWA MAKINI MAELEKEZO/MAAGIZO HAYA NA KUYATEKELEZA KIKAMILIFU.

KARIBU KATIKA SHULE HII.

.....
YOLANDA, N. MGATA

MKUU WA SHULE.

HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOLO
SHULE YA SEKONDARI DABAGA
FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA SHULE NA MASHARTI YAKE

A. MWANAFUNZI

Mimi nimesoma kwa makini barua ya maagizo ya kujiunga na shule pamoja na taratibu zake. Kwa heshima na unyenyekevu mkubwa ninakubali nafasi hii na nitafuata taratibu, kanuni, na sheria za shule hii.

B. MZAZI/MLEZI

Mimi Mzazi/Mlezi wa ambaye amechaguliwa kujiunga na shule yako. Nimesoma maagizo ya kujiunga na shule na sheria zake. Hivyo, ninakubali nafasi hii. Na ninaahidi kumtimizia mtoto wangu maagizo yote ya kujiunga na shule hii katika muda uliopangwa. Pia nitashirikiana daima na shule yako katika kumkuza na kumlea mtoto wangu. Ahsante.

Jina la Mzazi/Mlezi;

Anwani;

Kitongoji/Mtaa;

SimuNamba;.....

Tarehe;Saini

Tanbihi;

- Mzazi/Mlezi akibadilisha anwani au kuhama atujulishe mara moja anwani mpya.

KILOLO DISTRICT COUNCIL
MEDICAL EXAMINATION FORM
DABAGA SECONDARY SCHOOL
P. O. BOX 285IRINGA

(To be completed by medical officer in respect of all form entrants.)

Full name;

Age;years. Sex;

Blood count (Red and White);

Stool examination;

Urine analysis;

Syphilis test;

Eye test;

T.B test;

Ears;

Chest;

Spleen;

Abdomen;

ADDITIONAL INFORMATION; (e.g Physical or Chronic family disease, etc.)

.....
.....

.....(Names) I certify that the above is fit/not fit to pursue studies.
Signature;

Designation;

Section;

Date; Official Stamp;

N.B: Note any others, at the time of medical examination of an individual.

Pupils: You must bring the complete form when you come to school. Pupils without certificate of physical fitness will not be accepted.

.....
YOLANDA, N. MGATA
THE HEAD OF SCHOOL